JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

## TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI MACHI NA APRILI, 2026

### 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwezi Machi na Aprili 2026, maeneo mengi nchini yaliendelea kupata mvua. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo katika mwezi Machi. Hali hii ilipelekea kuongezeka kwa unyevu ardhini, kuongezeka kwa kina cha maji na malisho katika baadhi ya maeneo; na kusababisha mafuriko, kutuama kwa maji, kuathiri shughuli za kiuchumi na uharibufu wa mali na miundombinu katika baadhi ya maeneo. Hali ya joto ya kawaida hadi joto kali ilijitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan yaliyokuwa na upungufu wa mvua. Aidha, vipindi vichache vya upepo mkali vilijitokeza katika maeneo ya ukanda wa pwani na ziwa Victoria.

Kwa ujumla, hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa ya mwelekeo wa misimu iliyotolewa.


### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Machi, 2026

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2026 vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo vilijitokeza katika maeneo mengi. Kuimarika kwa Ukanda mvua (ITCZ) pamoja na wimbianga (MJO) kulichangia uwepo wa vipindi vya mvua kubwa zilizoambatana na ngurumo. Hali hii iliweza kusababisha mafuriko, kutuama kwa maji, kuathiri shughuli za kiuchumi, uharibifu wa miundombinu na mali pamoja na vifo.
Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 144.9 kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa Kilwa (mkoa wa Lindi) mnamo tarehe 22 Machi, ikifuatiwa na milimita 117.0 katika kituo cha Moshi (mkoa wa Kilimanjaro) na milimita 110.0 katika kituo cha Lyamungo (mkoa wa Kilimanjaro) mnamo tarehe 1 na 20 Machi, 2026 mtawalia. Vituo vilivyopima mvua milimita 60 au zaidi ni kama inavyoonekana katika kielelezo Namba 1.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 02/2026*




**Kielelezo 1**: Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Machi 2026

Taarifa kutoka vyombo vya habari zilithibitisha athari mbaya za mvua na radi katika mwezi husika. Mnamo tarehe 10 Machi 2026, mvua kubwa iliyonyesha kwa muda mrefu katika mkoa wa Mwanza ilisababisha mafuriko katika maeneo kadhaa, na kuathiri kwa kiasi kikubwa usafiri na shughuli za kiuchumi. Katika tukio jingine tarehe 18 Machi 2026, katika eneo la Kivule, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, wanafunzi watatu wa Shule ya Msingi Msongola walipoteza maisha huku wengine wawili wakijeruhiwa baada ya kupigwa na radi.



**Kielelezo 2:** Magari yakiwa yamezingirwa na maji ya mafuriko katika eneo la Mkuyuni, Mwanza, kufuatia mvua kubwa iliyosababisha mafuriko makubwa alfajiri ya tarehe 10 Machi 2026 (Chanzo: Star TV Africa).

**1.2 Hali joto kwa mwezi Machi, 2026**

Katika mwezi wa Machi 2026, hali ya joto la wastani hadi kali ilijitokeza katika maeneo machache nchini, hususan ukanda wa pwani na nyanda za juu za kaskazini-mashariki.

Wakati wa mchana, viwango vya juu vya joto vilionyesha ongezeko dogo katika baadhi ya maeneo ya nchi. Kiwango cha juu zaidi cha joto, 35.2 °C, kilirekodiwa katika kituo cha Mlingano (Mkoa wa Tanga) tarehe 19 Machi, kikifuatiwa na nyuzi joto 34.2 °C zilizorekodiwa katika kituo cha Zanzibar tarehe 2 Machi 2026.

**1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Septemba, 2026**


Katika mwezi Machi 2026, upepo wa kawaida uitawala katika maeneo mengi. Hakukua na vipindi vya upepo mkali unaozidi kilomita 40 kwa saa.

**1.4 Mvua kubwa kwa mwezi Aprili, 2026**

Katika mwezi wa Aprili 2026, mvua zilizoambatana na radi zilishuhudiwa katika baadhi ya maeneo ya nchi, huku vituo kadhaa vikirekodi mvua kubwa ya angalau milimita 50 ndani ya saa 24. Kiwango kikubwa zaidi cha mvua kilichorekodiwa katika mwezi huu kilikuwa milimita 126.9 mnamo tarehe 13 Aprili 2026 katika kituo cha Mlingano (Mkoa

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

wa Tanga), kikifuatiwa na milimita 100.6 na 96.7 zilizorekodiwa tarehe 4 na 6 Aprili katika vituo vya Kigoma na Mahenge (Mkoa wa Morogoro), mtawalia. Vituo vilivyorekodi kiasi cha mvua cha milimita 60 au zaidi vimeoneshwa katika Kielelezo 3.




**Kielelezo 2:** Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Aprili, 2026

Mvua kubwa iliyonyesha usiku wa kuamkia tarehe 6 Aprili 2026 mkoani Kigoma iliathiri zaidi ya kaya 135, huku kaya 20 kati ya hizo zikibaki bila makazi kabisa baada ya nyumba zao kubomolewa.




**Kielelezo 4:** Uharibifu wa nyumba uliosababishwa na mvua kubwa iliyonyesha usiku wa kuamkia tarehe 6 Aprili 2026 mkoani Kigoma (Chanzo: Azam TV).

**1.5 Hali joto kwa mwezi Aprili, 2026**

Katika mwezi wa Aprili 2026, hali ya joto la juu la kawaida ilitawala katika baadhi ya maeneo ya nchi, huku kiwango cha juu zaidi cha joto kilikuwa nyuzi joto 34.6 °C kilichorekodiwa katika kituo cha Kibaha (Mkoa wa Pwani) mnamo tarehe 4 Aprili 2026. Katika mwezi huu, hakukuwa na viwango vya vya joto kali zaidi vilivyorekodiwa.

Hata hivyo, viwango vya chini zaidi vya joto (baridi kali ) vilirekodiwa katika maeneo machache ya nyanda za juu kusini-magharibi, hususan Mkoa wa Njombe. Kituo cha Igeri kilirekodi kiwango cha chini zaidi cha joto cha nyuzi joto 9.9 °C tarehe 11 Aprili, kikifuatiwa na nyuzi joto 10 °C tarehe 5 Aprili 2026.

**1.6 Upepo Mkali kwa mwezi Aprili, 2026**

Katika kipindi cha mwezi Aprili, vipindi vya upepo mkali, wenye kasi ya kilomita 40 kwa saa vilijitokeza katika maeneo machache, ikiwemo maeneo ya ukanda wa pwani na ziwa Victoria.

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 15 Mei, 2026*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz